



# **GRE TSA UNIVERSITY - THIKA**

## **UNIVERSITY EXAMINATIONS JANUARY - APRIL 2025 SEMESTER**

### **DIPLOMA IN EDUCATION (ARTS)**

**KODI: DKIS 014**

**KOZI: MOFOLOJIA YA KISWAHILI**

**TAREHE: APRILI 2025**

**WAKATI: SAA 2**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

1. SEHEMU YA KWANZA **A**: NI YA **LAZIMA**
2. SEHEMU YA PILI **B**: JIBU MASWALI YOYOTE **MAWILI**
3. **USIANDIKE CHOCHOTE** KWENYE KARATASI YA MTIHANI. KWA KUFANYA HIVYO UTAKUWA UMEVUNJA SHERIA ZA MITIHANI NA UTAADHIBIWA
4. **ANDIKA VIDOKEZO VYAKO NYUMA YA KIJITABU CHA MAJIBU KISHA PIGIA MSTARI BAADAYE**

**TAHADHARI:**-kamera za CCTV zipo kwenye vyumba vyote vya mitihani

## **SEHEMU YA A: YA LAZIMA**

### **SWALI LA KWANZA**

- a) Eleza dhana zifuatazo:
- i. Mofolojia [Alama 2]
  - ii. Neno changamano kimofolojia [Alama 2]
  - iii. Alomofu [Alama 2]
  - iv. Mofu [Alama 2]
- b) Bainisha mofu zilizomo katika maneno yafuatayo:
- i. Wanajiimbia [Alama 3]
  - ii. Somo [Alama 2]
  - iii. Mpishi [Alama 2]
  - iv. Huku [Alama 2]
- c) Jadili tofauti nne zilizopo kati ya mofolojia ya uambishaji na ile ya unyambuaji. [Alama 13]
- 

## **SEHEMU YA B: YAJIBU MASWALI YOYOTE MAWILI**

### **SWALI LA PILI**

- a) Fafanua dhana zifuatazo:
- i. Umbo-neno [Alama 4]
  - ii. Leksimu [Alama 4]
- b) Eleza aina tatu za mofu kulingana na kigezo cha kimuundo. [Alama 12]
- ### **SWALI LA TATU**
- a) Bainisha miundo minne ya nomino za Kiswahili. [Alama 12]
- b) Bainisha viambishi vya unyambuaji katika Kiswahili. [Alama 8]

### **SWALI LA NNE**

- a) Fafanua mofimu zinazowakilishwa na mofu zinazopachikwa kabla ya mzizi wa kitenzi. [Alama 12]
- b) Eleza mbinu mbili za uundaji wa msamiati mpya katika Kiswahili. [Alama 8]

### **SWALI LA TANO**

- a) Jadili uainishaji wa kimofolojia wa ngeli za nomino za Kiswahili. [Alama 12]
- b) Fafanua umuhimu wa uambishaji katika Kiswahili. [Alama 8]